# MWAKA WA 2022 UWE NI MWAKA WA KILA MTEULE KUJISIFIA WOKOVU NA SIYO KITU KINGINE KAMWE!!!!
# MAANDIKO: YER. 9: 23 – 24.

1. Bwana mwenyewe aliamua kumjulisha Nabii Yeremia siri hii kubwa ambayo wateule wengi hatujui hata leo kwamba iko haja ya wateule kujisifu baada ya kuwa na hakika kwamba uhusiano wetu na Bwana Yesu uko sawasawa.

- Hata mara moja mteule hatakiwi kujivunia maarifa haya ya kidunia au uwezo alionao wa kibinadamu**,** au hata utajiri huu wa kidunia unaoonekana kwa macho haya ya nyama!! Thamani zote za vitu vya kidunia "**hupauka"** (hupoteza umuhimu wake; hupoteza mvuto wake pale aliye navyo anapokuwa hamchi Mungu (hana maarifa ya Mungu; **Pale mtu anaposhindwa kujali kwa ndani sana ya moyo wake heshima na hadhi ya Mungu; thamani ya vitu vingine vyote alivyonavyo inakosa maana**. (Neno zuri lililotumika katika Biblia ya Amplified ni "***Let not the wise and skillful person BOAST in his wisdom and skill, let not the mighty and powerful person boast in his strength and power; let not the person who is rich in physical gratification and earthly wealth boast in his temporal satisfactions and earthly riches. Yer. 9: 23!***
- **Kwa maana hasa ya Ki-Mungu:-**
  a. Kuna (kujisifu/kujigamba) kuzuri (pale unapojisifia /unapojigambia) ukuu na uwezo wa Mungu wako.

  b. Kunakujisifu/kujigamba kubaya pale unapojisifia/ unapojigambia uwezo ulionao, maarifa au utajiri ulionao kwa kuamini kwamba umefika hapo ulipo kwa nguvu zako na juhudi zako.

## 2. <u>Mifano yawatu waliojisifu mbele za Bwana vyema.</u>

**a. Nabii Eliya- 1Wafal. 17: 1, 18: 17 – 46.**

Nabii Eliya kama mjumbe wa Mungu duniani, alisema Neno la hukumu kutoka kwa Mungu juu ya Israel ilipokuwa imeasi na Mungu akazuia mvua kwa muda wa **miaka $3^1/_2$.** Nabii anajisifia Mungu wa Israeli tofauti na Mfalme Ahabu ambaye anajisifia Baali.

- Neno hili la hukumu pia lilikuwa linamdhihaki Baali ambaye waliokuwa wanamwabudu walikuwa wanamwamini kwamba ndiye anayetawala mvua na kwamba yeye ndiye aliyekuwa na uwezo wa kuleta mazao katika Nchi!! Ndiyo maana Nabii Eliya alitamba pamoja na kuwadhihaki!! Maana baali alishindwa kuleta mvua kwa **miaka $3^1/_2$** na pia alishindwa kushusha moto walipomwita siku mzima.

- Nabii Eliya alifahamu kwamba Mungu pekee ndiye aliye na uwezo wa kuleta mvua tena kwa wakati ili wapate kuvuna nafaka. ***Kumb. 11: 13 - 15.***

b. **Kijana Daudi. 1Samwl. 17: 26, 32 – 37, 45 - 54; 2Samwl. 7: 1 – 2**.

- **Daudi alikuwa na moyo wa kujali kwa ndani sana heshima na hadhi ya Mungu wa Israeli** (**mst. 26, 36, 46**).
- Yeye alitambua kwamba Goliathi hawatukani tu majeshi ya wana wa Israeli; bali zaidi sana alitambua kwamba anamtukana na kumkashifu Mungu wa Israeli.
- Daudi hakujisifia/hakutamba au hakujiamini kwa sababu ana hekima au silaha nzuri au ana uwezo fulani bali alijisifu/alitamba kwa sababu anamjua Mungu pamoja na uwezo wake **– Mst. 37, 45-47. Soma pia Zab. 33: 16 – 17, Zab. 44: 1-8 * (6-8). (**Kama ni kiwango cha elimu na maarifa ya dunia hii, Daudi alikuwa hana maana mpaka anapakwa mafuta na nabii Samweli, yeye alikuwa ni mchungaji wa kondoo wa baba yake tu. ***1Samwl. 16: 11 – 13.***

- **<u>Nabii Elisha. 2Wafal. 5: 1 – 7, 8-16</u>.** Wakati Mfalme wa Israel anahaha asijue cha kufanya juu ya jemedari Naamani na ukoma wake na kudhania kwamba huo ulikuwa ni uchokozi tu wa mfalme wa Shamu wa kutaka kuanzisha vita na Israel; Elisha anasimama na kumwambia Mfalme **"mbona umeyararua mavazi yako? Na aje sasa kwangu mimi, naye atajua ya kuwa yuko nabii katika Israeli. (Tambo za Nabii Elisha hizo!!! Na aje kwangu naye atajua!!**)

  Nabii Elisha kumwambia Jemedari Naamani akaoge katika maji yaliyojaa tope (Yordani) alikuwa anataka kuona **kama Naamani ana moyo wa unyenyekevu na utii anapokuja mbele za Mungu kama ambavyo na yeye Askari walio chini yake wanapokuja mbele yake sharti wawe wanyenyekevu na watii**.

- Maji haya haya yaliyo na tope nyingi ndiyo yakatumiwa kuponya mwili wa Jemedari Naamani na akamwamini Mungu wa Israeli – ***mst. 15 – 16;*** na hata Mfalme wa Israeli kwa vyovyote alishangaa kwa sababu wakati huo Israeli ilikuwa na wakoma wengi tu ambao walifahamu kwamba mto Yordani usingeweza kuwa suluhisho la wao kuponywa ukoma wao.

- ***2Wafal. 7: 1 – 2;*** Wakati Nchi imeingia katika shida ya njaa kubwa (**2Wafal. 6: 24 – 33)** Elisha anasimama na kusema/kutabiri kwamba ule uhaba wa chakula utakwisha kesho na bei ya chakula itashuka na kuwa bei poa!! **(wamjuao Mungu wao ndugu watatenda makuu. Dan. 11:32.**

- Haya ni maneno ambayo yalimchanganya kabisa Akida wa Mfalme, lakini kesho yake unga ukauzwa bei poa sawasawa na Neno la Nabii*- **2Wafal. 7: 16.***

  "Kujisifu kwa sababu ya Bwana (kutamba) siyo Dhambi au kuonyesha kiburi la hasha; Bwana mwenyewe anawafurahia watumishi wa jinsi hii na kuwaunga mkono. ***2Kor. 10:17; 1Kor. 1: 31.*** (**kuona fahari kwa sababu ya Bwana ni sawa kabisa. Mwanzo 45: 4 – 13.**

**<u>3. Mifano ya watu waliojisifia uwezo/hekima/utajiri wao.</u>**

a. **<u>Mfalme Nebukadreza</u>**: ***Dan. 4: 28 – 37***. Hadi hapo Mfalme Nebkadreza fahamu zake zilipomrudia na kisha kutambua kwamba bila nguvu na uweza wa Mungu kumwezesha; yeye asingeweza kutawala wala kufanya yote aliyokuwa ameyafanya; ndipo alipopata rehema na kufundisha wengine waliokuwa na tabia kama yake.

**b. <u>Mfalme Herode: Mdo. 12: 21 – 23</u>**- Pale mtu anapojaribu tu kugusa utukufu wa Mungu ili uwe wake; Mungu hawezi kukubali kamwe- ***Isaya 42: 8, Luk. 12: 13 – 21;*** "**unajua kujivunia/kujisifia mali za dunia hii, hekima, uwezo na utajiri katika maisha haya ya dunia hii ni kosa kubwa sana mbele za Mungu. Hakuna aliiyekuja navyo saa anazaliwa.** ***Ayub. 1: 20 – 22.***

***Note:*** **Ni vizuri na bora zaidi kutafuta kuwa matajiri na wenye hekima zaidi kwa Mungu wetu kwanza kwa kuutafuta ufalme wake kwanza pamoja na haki yake.** ***Math. 6:33,*** **ndipo tutakapokuwa sababu ya kujisifu/kujigamba mbele za Bwana siku zote za maisha yetu hapa duniani**.

**4. Mwaka 2022** Bwana anataka kuona wateule walio na moyo wa kujali kwa ndani sana heshima na hadhi yake ili apate kuwatumia kwa viwango vikubwa katika kuleta mabadiliko ambayo yanasababisha Jina lake lisitukamwe tena ***Amina.***

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***09/01/2022***